JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BARAZA LA MITIHANI

MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A

652 **ELIMU KWA MICHEZO**

Muda: Saa 3. **Mwaka : 2012**

MAELEKEZO.

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C** yenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu **B** and **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** na **C** zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Vikokotozi **haviruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

SEHEMU A (40 Alama)

Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. Eleza maana ya rasilimali fedha katika michezo na umuhimu wake.
2. Taja michezo minne ya asili inayoweza kufundishwa shuleni na eleza lengo la kila mchezo.
3. Fafanua hatua nne za kufuata wakati wa kutoa pasi katika mpira wa kikapu.
4. Eleza sheria nne kuu zinazopaswa kuzingatiwa katika mchezo wa tenisi ya meza.
5. Changanua stadi nne muhimu katika mchezo wa netiboli.
6. Eleza faida nne zinazopatikana kwa wanafunzi wanapojitolea kusimamia mashindano ya michezo shuleni.
7. Eleza stadi nne zinazohitajika ili kufunga goli kwa ufanisi katika mpira wa mikono.
8. Bainisha faida nne za kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano katika michezo ya shule.
9. Eleza mambo manne muhimu ya kuzingatia katika kuandaa mashindano ya michezo ya shule ya sekondari.
10. Eleza njia nne ambazo waamuzi hutumia kufikisha maelekezo yao kwa wachezaji wakati wa mchezo.

SEHEMU B (30 Alama)

Jibu maswali mawili katika sehemu hii

11. Eleza sababu tano zinazofanya michezo kuwa nyenzo ya kuimarisha mshikamano wa kikabila.
12. Changanua hatua tano zinazopaswa kufuatwa wakati wa kutoa huduma ya kwanza kwa mchezaji aliyeumia kifundo cha mguu.
13. Fafanua mifumo mitatu ya wachezaji katika mpira wa miguu na faida za kila mfumo.

SEHEMU C (30 Alama)

Jibu maswali mawili katika sehemu hii

14. Eleza kanuni sita za usalama zinazopaswa kuzingatiwa katika michezo ya riadha.

15. Tathmini changamoto zinazojitokeza katika usimamizi wa mashindano ya michezo ya shule na namna ya kuzitatua.

16. Kwa mifano, eleza nafasi ya teknolojia ya mawasiliano katika kukuza michezo kitaifa na kimataifa.